

Mwafrika

3/8/63

UNO NA MRENO

BARAZA la Usalama la Umoja wa Mataifa mjini New York limekubaliana na azimio la nchi za Afrika na Asia kwamba Mreno aache kabisa tabia yake ya kuwakandamiza wananchi walioko katika nchi anazotawala Afrika. Pia awatayarishe kujitawala. Azimio hilo pia limeomba nchi nyingine zisimuuzie silaha.

Uingereza, Amerika na Ufaransa hazikupiga kura. Sababu kubwa ya nchi hizi tatu kukataa kupiga kura ni wazi. Wanaogopa kumuudhi mwanachama mwenzao katika umoja wa NATO.

Lakini hiyo ni kazi bure, kwasababu wao wenyewe wameziachia nchi walizokuwa wakizitawala. Haku-na sababu basi wamsaidie mtu ambae ana nia ya kuwakandamiza watu wengine.

Hata hivyo azimio hilo limekwisha kupita na kitu kilichobaki ni kwa Umoja huo wa Mataifa kuchukua hatua ya kutimiza azimio hilo.

Nchi za Uingereza, Amerika na Ufaransa lazima zikumbuke kwamba kujitahidi kwao kumpa au kumuuzia zana za vita Mreno, hakutasaidia kitu, kwasababu kufanya hivyo ni kuhatarisha kabisa amani ya Ulimwengu.

Nchi za Afrika hazitakubali kunyamaza kimya tu na kuona ndugu zao wanakandamizwa na kutawaliwa kwa nguvu na watu walioko maili elfu nyingi.

Ikiwa Mreno na wote wanaohusika na kumsaidia Mreno watakataa kutimiza maazimio ya Umoja wa Mataifa, basi nchi ya Afrika itaweka maazimio vake yenyewe na kuchukua hatua ambayo wanaona inastahili.

Kuzuia haya yasitokee itakuwa busara kwa nchi zote za ulimwengu kufuata maazimio ya UNO na kudemisha amani ya ulimwengu.

M.P. Shis